JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

05 **SAYANSI**

MUDA: Saa 1½ **Asubuhi tarehe 13/09/2007**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina maswali 50 katika sehemu A na B.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Majibu **yote** yaandikwe katika karatasi ya kujibia uliyopewa.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika karatasi ya kujibia.

SM Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.

Scanned with CamScanner

SEHEMU A

Chagua jibu sahihi kisha andika herufi inayohusika mbele ya namba ya kila swali katika karatasi ya kujibia.

1. Umuhimu wa vyakula vya kabohaidreti mwilini ni _____.
   A kujenga mwili
   B kulinda mwili
   C kutia nguvu
   D kuweza kufikiri
   E kuongeza joto.

2. Ukiwa katika chumba chenye giza na ghafla taa ikawashwa, kitatokea nini kuhusu jicho?
   A Mboni ya jicho itaongezeka ukubwa.
   B Mboni ya jicho itabaki vilevile.
   C Lenzi ya jicho itabinuka.
   D Mboni ya jicho itapungua ukubwa.
   E Kelele za nguvu zitasikika.

3. Kikohozi kikavu, homa, kutoka jasho usiku na kukohoa damu ni dalili za _____.
   A Kifua kikuu
   B Tetekuwanga
   C Pepopunda
   D Homa ya matumbo
   E Kifaduro.

4. Michoro katika kielelezo namba 1 inawakilisha seli katika mwili wa binadamu ambazo kazi zake ni _____.
   A kuzuia na kukinga maradhi mwilini
   B kusafirisha oksijeni
   C kugandisha damu
   D kurekebisha joto la mwili
   E kusafirisha taka mwilini.



Kielelezo na 1.

5. Mtu mwenye kiribatumbo ni rahisi zaidi kupata ugonjwa gani?
   A Moyo na msukumo mkubwa wa damu.
   B Kansa
   C Unyafuzi
   D Kuvia kwa ukuaji wa akili
   E Kwashakoo.

SM

Scanned with CamScanner

6. Vinyesi na vitu vya wanyama na mimea vilivyooza _____.
   A huufanya udongo usifae kwa kilimo
   B vinakaribisha wadudu wengine wanaoharibu mazao
   C vinaongeza mbolea ya mboji kwenye udongo
   D havina umuhimu katika udongo
   E vinatumika kama chambo kwa wavuvi.

7. Mwanga na sauti vina tabia zinazofanana isipokuwa tabia moja tu. Je tabia hiyo ni ipi?
   A Kupinda B Kuakisiwa C Kusharabiwa
   D Kupita kwenye vakyumu E Kusambaa.

8. Kuhifadhi vyakula katika jokofu ni njia ambayo _____.
   A hufanya vyakula vikae muda mrefu bila kuharibika
   B inapunguza kazi ya kupika mara kwa mara
   C inapoteza ladha na kuvifanya vioze iwapo vitakaa siku nyingi
   D hugeuza chakula kuwa barafu
   E inapunguza gharama ya kwenda sokoni.

9. Ukiweka sarafu ya shilingi 20 katika beseni lenye maji, sarafu hiyo inaonekana imepanda juu. Hali hiyo hutokea kwa sababu _____.
   A sarafu hiyo ni nyepesi
   B macho yana matatizo
   C mwanga umenyooka
   D maji ni kidogo
   E mwali wa mwanga hupinda unapoingia katika maji.

10. Kwa nini chupa ya soda na bia hazijazwi hadi pomoni?
   A Kwa ajili ya nafasi ya gesi.
   B Husaidia kufungwa chupa kwa urahisi.
   C Kuruhusu kutanuka wakati wa hali ya hewa ya joto.
   D Kupunguza gharama.
   E Ikijazwa huweza kumwagikia mnywaji.

11. Volcano hai hutoa kimiminika kizito katika uso wa dunia kiitwacho _____.
   A Lava B Kreta C Gesi
   D Volcano E Maji.

12. Kwa nini kwa kawaida mwanga unaonekana kwanza kabla ya mngurumo wa radi ingawa vyote vinatokea pamoja?
   A Mwanga una mawimbi makubwa kuliko sauti.
   B Mishipa ya fahamu ya macho inafanya kazi haraka kuliko mishipa ya fahamu ya kusikia.
   C Mwendokasi wa mwanga ni wa haraka kuliko wa sauti.
   D Mwanga na sauti kwa kawaida husafiri wima.
   E Mawimbi ya sauti hayasafiri katika hewa.

Scanned with CamScanner

13. Kipi kati ya vitu vifuatavyo vinaweza kusababisha uchafuzi wa hewa?
A Maji machafu ya viwandani, spiriti na ujenzi wa barabara.
B Moshi, majivu na mbolea.
C Moshi wa viwandani na matokeo ya kuungua kwa petroli.
D Misitu ya asili, viwanda na mbolea.
E Mbolea, mboji na maji machafu ya viwandani.

14. Ni kiumbe yupi kati ya vifuatavyo huishi kwenye maji?
A Inzi. B Buibui. C Kaa.
D Panzi. E Mende.

15. Ukuaji wa mbu hupitia katika hatua kuu nne. Mtiririko sahihi wa ukuaji huo ni _____.
A yai, pupa, lava, mbu B pupa, yai, lava, mbu
C yai, lava, pupa, mbu D lava, yai, pupa, mbu
E pupa, lava, yai, mbu.

16. Kitendo cha mmea kufuata mwanga katika kielelezo namba 2 huitwa _____.



Kielelezo namba 2

A kutembea B kukua C kujongea
D kuitikia kichocheo E kuhisi.

17. Chanzo cha chakula kwa wanyama ni _____.
A mimea B mimea na nyama
C mimea kwa hebivora na nyama kwa canivora
D maziwa E maharage.

18. Vyombo vya kupikia vina mikono iliyotengenezwa kwa mbao na plastiki kwa sababu _____.
A haipitishi joto haraka B haipitishi joto
C husharabu joto D huakisi joto
E hutunza joto kwa muda mrefu.

Scanned with CamScanner

19. Kuta, sakafu na dari ya vyumba vya utangazaji vimewekwa vitu laini ili _____.
A kupunguza sauti
B kuakisi sauti
C kuongeza sauti na nguvu
D kufanya sauti kuwa laini na safi
E kupunguza mwangwi.

20. Kuna uhusiano gani kati ya sumaku na umeme?
A Zote ni nishati za kemikali.
B Zote ni sakiti za umeme.
C Kuliko na sumaku lazima kuwa na umeme.
D Kuliko na umeme lazima kuwa na sumaku.
E Zote zinatoa nishati ya mwanga.

21. Katika mchoro wa sakiti ya umeme, alama  inawakilisha ____.
A seli kavu
B seli
C fyuzi
D transfoma
E adapta.

22. Ni kundi lipi linawakilisha mashine rahisi?
A Nyundo, shoka, kisu na mkasi.
B Mkasi, gari, toroli na msumari.
C Shoka, skrubu, mkasi na cherehani.
D Kitasa, toroli, baiskeli na msumeno.
E Baiskeli, gari, cherehani na nyundo.

23. Wakati mtu anasukuma toroli, mikono yake na mishikio ya toroli inafanya _____.
A egemeo
B mzigo
C jitihada
D nyenzo
E nishati.

24. Dira huelekea upande wa kaskazini wa dunia kwa sababu _____.
A kuna nguvu ya sumaku ndani ya dunia inayoingiliana
B watu wamezoea zaidi ncha ya kaskazini
C sio rahisi kupotea kama upo ncha ya kaskazini
D wayumbuzi wa mwanzo waligundua zaidi ncha ya kaskazini
E ncha ya kaskazini iko juu kuliko ncha ya kusini.

25. Ni mabadiliko gani yatatokea kama mtu akipumulia kwenye uso wa kioo?
A Kuganda.
B Kuyeyuka.
C Kuvukizwa.
D Mtonesho.
E Kutanuka.

26. Vinundu vilivyoko kwenye mimea jamii ya mkunde vina bacteria ambao husharabu na kubadili _____ kuwa naitreti.
A naitrojeni
B yurea
C fosforasi
D haidrojeni
E salfeti ya Ammonia.

Scanned with CamScanner

27. Chunguza kwa makini kielelezo namba 3 na kisha jibu swali linalofuata:



Kielelezo namba 3

Kabla ya kutumbukiza jiwe Baada ya kutumbukiza jiwe

Nini ujazo wa jiwe baada ya kutumbukiza katika maji?

A Sm^3 15. B Sm^3 45. C Sm^3 30.
D Sm^3 5. E Sm^3 20.

28. Myeyuko wa majivu yaliyotokana na majani ya mgomba huweza kubadili karatasi ya litmas ya _____.

A bluu kuwa nyekundu B nyekundu kuwa bluu
C bluu kuwa njano D nyekundu E bluu.

29. Ripoti ya jaribio la kisayansi huandikwa kwa mpangilio ufuatao:

A Njia, vifaa, kusudi, matokeo, hitimisho
B Njia, vifaa, kusudi, hitimisho, matokeo
C Njia, vifaa, matokeo, kusudi, hitimisho
D Kusudi, njia, vifaa, matokeo, hitimisho
E Kusudi, vifaa, njia, matokeo, hitimisho.

30. Tezi lililo katika ubongo linalofanya kazi ya kuchochea tezi zingine kufanya kazi huitwa _____.

A kongosho B gonadi C tezi ya adrenali
D tezi ya thairoidi E tezi ya pituitary.

31. Ni ipi kati ya mishipa ya damu ifuatayo hupeleka damu kwenye mapafu?

A Vena Kaya. B Ateri ya pulmonary.
C Aota. D Vena ya pulmonary. E Vena ya renali.

32. Chembe nyekundu za damu hutengenezwa katika sehemu gani ya mwili?

A Uroto mwekundu wa damu.
B Moyo. C Tumbo. D Ini. E Mapafu.

Scanned with CamScanner

33. Ipi njia bora ya asili ya uzazi wa mpango?
A Kutumia kondomu wakati wa kujamiiana.
B Kutumia njia ya kitanzi.
C Kutumia sindano.
D Kutumia vidonge vya uzazi wa majira.
E Kutojamiiana katika kipindi cha hatari.

34. Sehemu ya mbegu ambayo huhifadhi chakula cha mmea kwenye udongo ni ____.
A embryo B testa C kotiledoni
D epikapi E kianza mche.

35. Mayai ya kike hutengenezwa kwenye _____.
A korodani B mirija ya falopia C uterasi
D ovari E mlango wa uzazi.

36. Matokeo ya mwisho ya myeyusho wa protini ni _____.
A asidi za fati na gliserini B asidi za amino
C glukosi D asidi ya haidrokloriki
E sukari laini.

37. Sehemu ya ua ambayo ni sawa na ogani ya uzazi ya kike katika mwili wa binadamu ni _____.
A stigima B stameni C ovyuli
D ovari E staili.

38. Tunashauriwa kupanda miti kwa wingi sehemu zilizo kame ili _____.
A kuzuia mmomonyoko wa udongo
B kuleta kivuli
C kupata kuni
D kupata mbao na matunda
E kusaidia kuleta mvua.

39. Watu waishio katika sehemu za baridi hupaswa kula zaidi vyakula aina ya mafuta kwa sababu vyakula hivyo _____.
A hulinda mwili B hujenga mwili C huleta joto
D hutuliza njaa E huleta nguvu.

40. Tunapopiga picha kwa kutumia kamera tunatumia moja ya sifa za mwanga. Sifa hiyo ni _____.
A kuakisiwa kwa mwanga
B mwanga kusafiri katika mstari mnyoofu
C kupinda kwa mwanga
D kusambaa kwa mwanga
E kusharabiwa kwa mwanga.

Scanned with CamScanner

41. Pau (Ethi) la radi hutengenezwa kwa shaba kwa sababu shaba _____.
A haipati kutu
B hupitisha umeme
C haiathiriwi na maji
D hupambana kirahisi na kemikali
E rangi yake haichuji.

42. Ni ugonjwa upi kati ya magonjwa yafuatayo unaweza kumpata mtu kwa kula nyama ambayo haikuiva?
A Punye. B Kwashakoo. C Tegu.
D Malaria. E Unyafuzi.

43. Kipi kati ya vifuatavyo husababisha kansa ya mapafu?
A Kuvuta tumbaku.
B Kunywa bia.
C Chanjo dhidi ya kipindupindu.
D Kunywa chai.
E Kunywa soda.

44. Iwapo mtu akitegemea sana pombe na hawezi kuiacha, ana tatizo la hali ijulikanayo kama _____.
A utapiamlo
B ulevi wa kupindukia
C kuzimia
D ugonjwa unaoua seli za ini
E unyong'onyefu.

45. Nini kati ya vifuatavyo ni chanzo kikuu cha vitamini C?
A Jibini. B Machungwa. C Maharage.
D Nyama. E Mayai.

SEHEMU B

Jibu maswali 46 – 50 kwa kuandika neno moja tu kwa kila swali katika karatasi yako ya kujibia.

46. _____ ni aina ya mbu anayeeneza malaria.

47. Virusi vya UKIMWI vinashambulia chembechembe _____ za damu katika mwili wa binadamu.

48. Kifaa kitumikacho kupima mwendokasi wa upepo kinaitwa _____.

49. Katika mlishano, mimea ya kijani inaitwa _____.

50. _____ ni minyoo midogo inayosababisha matende ambayo huenezwa na mbu aina ya kuleksi.

Scanned with CamScanner